JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26

**DODOMA** **12 JUNI 2025**

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26**

## UTANGULIZI

***1.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26. Pamoja na hotuba hii ninawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26. Taarifa hizi mbili ndiyo msingi wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2025/26 ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataiwasilisha katika Bunge lako Tukufu baadaye leo alasiri.

***2.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Tumeaaswa kuwa kila tunapopata fursa hatuna budi kumshukuru Mungu, na kuwashukuru watu ambao wameleta tofauti katika maisha yetu. Ninamshukuru Mungu kwa wingi wa rehema, baraka na fadhila zake kwangu iliyoniwezesha kusimama hapa mbele kuwasilisha Hotuba hii.

***3.*** ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, nafasi ambayo leo imenipa fursa ya kusimama hapa mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Hotuba hii. Ninamshukuru pia Mheshimiwa

Rais kwa utulivu na hekima za uongozi ambazo Mwenyenzi Mungu amemjalia, pamoja na juhudi zake za dhati alizoziweka katika kuiendeleza nchi yetu ili tuweze kufikia malengo tuliojiwekea. Aidha, ninamshukuru **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini na jitihada zake kubwa anazozifanya katika kuendelea kuijenga Zanzibar yenye maendeleo makubwa.

***4.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kuwapongeza **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na **Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.)**, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa maelekezo na miongozo yao kwetu, na kazi kubwa wanazofanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuongoza nchi yetu vyema.

***5.*** ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kuchukua nafasi hii kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza vizuri sana Bunge hili la 12. Uongozi wako makini, umahiri wako katika kujua masuala mapana ya kibunge hapa nchini na duniani, kwa jinsi ambavyo unapenda kutenda haki kwa wabunge wote bila kujali hali na nafasi zao, na upendo wako kwa wabunge wenzako, ni mambo ambayo yataacha alama ya kudumu ya uongozi wako kwa Bunge hili. Bunge hili linakuhitaji, wabunge

hawa wanakuhitaji, watanzania wanakuhitaji, dunia inakuhitaji, na muhimu zaidi wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini wanakukuhitaji uendelee kuwa kiongozi wetu na kiongozi wao! Tunakuombea na kukutakia kila la heri katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu!

***6. Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa kuiongoza kamati hii muhimu kwa ustadi na hekima. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti kwa ushirikiano waliotupa na michango yao makini katika maandalizi ya Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango ya Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26.

***7. Mheshimiwa Spika*****,** Taarifa hii ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 ni ya mwisho katika kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26). Aidha, taarifa hii inakamilisha kipindi cha miaka minne tangu Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iingie madarakani mwaka 2021. Katika kipindi hiki, uchumi wa nchi yetu umeendelea kuimarika na kuhimili changamoto zilizojitokeza duniani, ikiwemo Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO).

***8.*** ***Mheshimiwa Spika***, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 imeandaliwa kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla (ikijumuisha ukuaji wa Pato la Taifa, mfumuko wa bei, thamani ya shilingi na ajira), tathmini ya maendeleo ya sekta mbalimbali kwa mwaka 2024/25, hali ya biashara na uwekezaji, changamoto pamoja na vihatarishi vilivyojitokeza.

***9.*** ***Mheshimiwa Spika***, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yamezingatia vipaumbele vya Serikali vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, pamoja na miongozo mingine ya kisera ya kitaifa na kikanda. Miongozi hii ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EAC) 2050, Dira ya Maendeleo ya Jumuia ya Kusini mwa Afrika (SADC) 2050, Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika na Malengo Endelevu ya Maendeleo 2030 ya Umoja wa Mataifa.

# MWENENDO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024

***Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda***

***10. Mheshimiwa Spika***, Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Aprili, 2025 kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imeendelea kupungua hadi kufikia asilimia 3.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023. Upungufu huo ulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari za utekelezaji wa sera za fedha za mataifa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kupunguza ukwasi na kuongeza riba ili kukabiliana na mfumuko wa bei, na migororo ya kisiasa hususan Ulaya Mashariki na Mashariki ya Kati. Aidha, taarifa ya IMF inaonesha kuwa ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kupungua na kufikia asilimia 2.8 kwa mwaka 2025.

***11. Mheshimiwa Spika,*** Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili, 2025 kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kwa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kilikuwa asilimia 1.5 na asilimia 3.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 5.2 na asilimia 3.9 mwaka 2023, mtawalia. Kupungua kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kulitokana na migogoro ya kisiasa ikiwemo migororo inayoendelea nchini DRC na Sudani Kusini ambapo kumekuwa na ukuaji hasi wa asilimia 27.6

kwa Sudani Kusini. Aidha, athari za mabadiliko ya tabianchi zimepunguza ukuaji wa uchumi kwenye baadhi ya nchi za jumuiya hizo ikiwemo Malawi, Msumbiji na Sudani Kusini kufuatia hali ya ukame na mafuriko ulioleta athari kubwa katika sekta za kilimo, miundombinu na maisha ya watu. Aidha, kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa jumuiya hizo kinatarajiwa kufikia asilimia 2.7 kwa EAC na asilimia 3.5 kwa SADC kwa mwaka 2025.

***12.*** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili 2025, mfumuko wa bei duniani ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2024 kutoka asilimia 6.7 mwaka 2023. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulitokana na utekelezaji wa sera za fedha za kupunguza ukwasi na kushuka kwa bei za bidhaa muhimu hususan mafuta na mbolea katika soko la dunia. Mfumuko huu unatarajiwa kuendelea kupungua na kufikia asilimia 4.3 mwaka 2025 na asilimia 2.2 mwaka 2026.

***13.*** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 23.45 mwaka 2024 kutoka asilimia 15.5 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa chakula kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la gharama za usafirishaji. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa wastani wa asilimia 62.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 52.4 mwaka 2023.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA

***14. Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024, Pato halisi la Taifa lilifikia shilingi trilioni 156.6 kutoka shilingi trilioni 148.5 mwaka 2023, sawa na ukuaji wa asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 5.1 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na jitihada mbalimbali za Serikali, sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo. Jitihada hizo ni pamoja kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere; kuendelea na utekelezaji endelevu wa miradi ya kimkakati na ya kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji; kuongezeka kwa mikopo ya sekta binafsi; usimamizi madhubuti wa sera za fedha; kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; na uwekezaji wa Serikali katika huduma za jamii hususan elimu, afya, maji na hifadhi ya jamii.

***15. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024, sekta tano ziliongoza kwa ukuaji: ***sanaa na burudani*** (17.1%), ***uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme*** (14.4%), ***habari na mawasiliano*** (14.3%), ***fedha na bima*** (13.8%) na ***afya*** (10.1%). Sekta tatu zilichangia takribani nusu ya pato la taifa. Sekta hizi ni ***kilimo*** (26.3%), ***ujenzi*** (12.8%) na ***uchimbaji wa madini na mawe*** (10.1%). Tunachohitaji kwa siku za usoni ni kuongeza tija zaidi kwenye uzalishaji ili kilimo kiwainue Watanzania wengi zaidi kimapato.

***16.*** ***Mheshimiwa Spika***, Mfumuko wa bei nchini ulipungua na kufikia asilimia 3.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2023. Mfumuko wa bei ulipungua kutokana na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kutengemaa kwa bei za mafuta katika soko la dunia na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani. Kiwango hiki cha mfumuko wa bei kipo ndani ya wigo wa lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya kutokuzidi asilimia 8.0 na kuwa kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0, mtawalia.

***17.*** ***Mheshimiwa Spika***, Utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia riba ya Benki Kuu ulikuwa wa kuridhisha na ulifanikiwa kuhakikisha kuwa riba ya siku saba (7) katika soko la fedha baina ya mabenki inakuwa tulivu, ndani ya wigo usiozidi asilimia mbili (2) chini au juu ya riba ya Benki Kuu. Hali hii inaashiria uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi kinachoendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi. Matokeo ya utekelezaji huo umepelekea riba za mikopo kwa ujumla zilipungua hadi wastani wa asilimia 15.47 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.75 mwaka 2023. Riba za amana ziliongezeka hadi kufikia asilimia 9.17 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 8.65 mwaka 2023.

***18.*** ***Mheshimiwa Spika***, Mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha ambapo mwaka 2024 ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia wastani wa asilimia 12.4. Sekta zilizoongoza kupokea mikopo hiyo ni

***kilimo*** (41%), ***uzalishaji viwandani*** (16.3%), ***mikopo katika shughuli binafsi*** (14.7%), ***uchukuzi na mawasiliano*** (13.2%), ***biashara*** (12.7%) na ***ujenzi*** (4.4%). Matokeo hayo yanaonesha mwelekeo chanya katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta mbalimbali nchini. Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, hususan katika sekta za kilimo, uzalishaji viwanda, shughuli binafsi na uchukuzi na mawasiliano, linaashiria uimarishaji wa mazingira ya biashara na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Hatua za kisera zilizolenga kupunguza viwango vya riba na kuongeza bajeti katika sekta muhimu hususan kilimo zimeonekana kuwa na matokeo chanya katika kuchochea ukuaji huo.

***19.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kwa asilimia 9.0 na kufikia wastani wa shilingi 2,610.5 kwa dola moja ya Marekani mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,395.7 mwaka 2023. Upungufu huo ulitokana na utekelezaji wa sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ukwasi uliofanywa na mataifa yaliyoendelea, ikiwemo Marekani kwa lengo la kukabiliana na mfumuko wa bei.

***20.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Mwaka 2024, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,546.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,440.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kiasi hiki kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na

huduma kwa kipindi cha miezi 4.4, ambayo ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.0.

***21.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Machi 2025, deni la Taifa lilifikia shilingi trilioni 107.7 kutoka shilingi trilioni 91.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 14.9. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 34.76 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 70.94. Ongezeko la deni lilitokana na Serikali kuendelea kupokea mikopo mipya kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji.

***22.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuzalisha fursa za ajira kutokana na mipango na mikakati ya maendeleo inayotekelezwa katika kukuza ajira nchini. Kwa kutumia tafsiri mpya ya Ajira inayosema “Ajira mpya hutokea pale mfanyakazi anapoajiriwa kujaza nafasi iliyo wazi au nafasi mpya iliyoundwa kutokana na ukuaji wa shughuli za taasisi au uboreshaji wa mgawanyo wa majukumu kwenye taasisi au kujiajiri katika sekta rasmi na isiyo rasmi”. Katika kipindi cha kuanzia Novemba 2020 hadi Februari 2025 jumla ya ajira 8,084,204 zilizalishwa, kwa mgawanyo wa ajira 1,047,179 (13%) katika sekta rasmi na ajira 7,037,024 ( 87%) katika sekta isiyo rasmi.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2025

***23.*** ***Mheshimiwa Spika***, Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa hadi kufikia asilimia 6.0 mwaka 2025 kutoka asilimia 5.5 ya mwaka 2024;

(ii) Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani (mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ) kufikia asilimia 16.7 ya Pato la Taifa ifikapo 2025/26 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.8 mwaka 2024/25;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.3 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2025/26 kutoka matarajio ya asilimia 12.8 mwaka 2024/25;

(v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 3.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2025/26 kutoka matarajio ya asilimia 3.4 mwaka 2024/25; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

***24.*** ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina ya taarifa ya Hali ya Uchumi yanapatikana katika Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha Mwaka 2024.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/25

***25.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2024/25 Bunge lilidhinisha jumla ya shilingi trilioni 15.944 (sawa na 32.3% ya Bajeti Kuu ya Serikali) kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo. Bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2024/25. kwa ujumla wake, katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Serikali ilitenga ilitenga jumla shilingi trilioni 80.076 kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo, ikiwa ni sawa na wastani wa asilimi 35 ya Bajeti Kuu ya Serikali (jumla ya TZS trilioni 229.652) katika kipindi hicho

***26.*** ***Mheshimiwa Spika***, Kupitia bajeti za maendeleo zilizoidhiniwa na Bunge lako tukufu katika kipindi cha Bunge hili na utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali, kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo, imeweza kuchochea ukuaji wa uchumi, uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi, kuimarisha na kupanua huduma za jamii, na kuboresha ustawi wa wananchi kwa ujumla. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i) Kuongeza uwezo wa kuzalisha umeme kutoka Megawati 2,138 zilizokuwepo mwezi Machi, 2024 hadi MW 4,031.71 Aprili 2025, sawa na ongezeko la asilimia 86.6. Kutokana na hatua hii, pamoja na mambo mengine, Serikali imeweza kufikisha huduma ya umeme kwa

vijiji vyote nchini.

ii) kuendelea kutekeleza mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa ili kuinua na kuimarisha usafirishaji wa abiria na bidhaa ndani ya nchi pamoja na kuunganisha Tanzania na nchi jirani. Hadi kufikia Desemba, 2024, utandazaji wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa umefikia km 680.38. Aidha, kuanza kwa huduma za usafirishaji wa abiria kutoka Dar es Saalam hadi Dodoma kumepunguza muda wa safari kutoka saa tisa (9) hadi saa tatu (3) na hivyo kuwezesha muda uliopunguzwa kutumika katika shughuli zingine za uzalishaji mali. Vilevile, abiria 1,330,208 wamesafirishwa na jumla ya watanzania 206,579 wamepata ajira katika utekelezaji wa mradi huu.

iii) Ujenzi wa daraja la kisasa la Kigongo – Busisi (JPM) lenye urefu wa KM 3.2 lililopo Mwanza ambapo utekelezaji wake umekamilika na Daraja hili linatarajiwa kuzinduliwa rasmi tarehe 19 Juni 2025

iv) Kukamilika kwa ujenzi wa madaraja ya juu ya Uhasibu na Chang'ombe katika jiji la Dar Es Salaam. Kukamilika kwa miradi hii kutachochea ukuaji wa uchumi, kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa zinazoingia nchini na zinazokwenda nchi jirani.

v) Kuongeza matumizi ya mbolea kutoka tani 580,623 mwaka 2022/23

hadi tani 840,714 mwaka 2023/24. Ongezeko hili linatokana na Serikali kuanzisha mpango wa ruzuku ya mbolea ambao umepunguza gharama kwa wakulima kwa asilimia 50. Matokeo chanya ya kuongezeka kwa matumizi ya mbolea ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kulikopelekea kuongezeka kwa utoshelevu wa chakula kufikia asilimia 128 mwaka 2024/25 kutoka asilimia 124 mwaka 2023/24 na kuchangia asilimia 65 ya malighafi za viwandani kwa mwaka 2024.

vi) kuongezeka kwa mchango wa viwanda katika ajira zote kutoka asilimia 8.1 mwaka 2023 hadi asilimia 12.8 mwaka 2024; na kuongezeka kwa mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya juu katika mauzo nje kutoka asilimia 25 mwaka 2023/24 hadi asilimia 36 mwaka 2024/25.

vii) Kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini kutoka watalii 3,784,214 mwaka 2023/24 hadi watalii 5,360,247 mwaka 2024/25. Aidha, mchango wa utalii katika fedha za kigeni umeongezeka kutoka asilimia 25 mwaka 2023/24 hadi kufikia asilimia 26 mwaka 2024/25.

viii) Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilisajili jumla ya miradi mipya 691 yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 7,997.06 na ambayo ilitarajiwa kuzalisha ajira mpya 298,257.

Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 35.8 ukilinganisha na miradi 509 iliyosajiliwa mwaka 2023/24 ikiwa na thamani ya dola za Kimarekani milioni 5,825.00 na iliyotarajiwa kuzalisha ajira mpya 130,202. Kati ya miradi 691 iliyosajiliwa kwa mwaka 2024/25, asilimia 32 inamilikiwa na watanzania pekee, asilimia 23 inamilikuwa kwa ubia katika ya watanzania na wageni, na asilimia 45 ya miradi inamilikiwa na wawekezaji wa kigeni.

ix) Kuongezeka idadi ya wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba na kujiunga kidato cha kwanza kutoka asilimia 48 mwaka 2019/20 hadi asilimia 70 mwaka 2024/25.

x) Kuimarisha kwa upatikanaji wa huduma za afya karibu na wananchi kwa kujenga zahanati 980, vituo vya afya 367, hospitali mpya za halmashauri 129, hospitali tano za rufaa za mikoa na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara pamoja na kukarabati hospitali kongwe 50 na kuboresha hospitali tisa za rufaa za mikoa. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa majengo 116 ya huduma za tiba za dharura na ajali na kuweka vifaa tiba vya kisasa na hivyo kuwezesha kuwa na mfumo wa huduma za dharura kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Hospitali za Halmashauri/Wilaya.

xi) Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ambapo idadi ya wananchi vijijini wanaopata huduma hii imefikia asilimia 79.7

mwaka 2024.

***27.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** mwelekeo wa muda mrefu wa sera za kiuchumi wa Chama Cha Mapinduzi ni kujenga uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea (yaani modenaizesheni ya uchumi) na kutekeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa lengo la kutokomeza umaskini.

***28.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Kuna hatua mbili kubwa za kuwawezesha wananchi kiuchumi. Mosi, ni kuweka mazingira ya wananchi kujitengenezea kipato kwa njia ya kuajiriwa, kujiajiri au biashara. Pili, ni Serikali kuwapunguzia wananchi gharama za maisha kwa kuwaondolea baadhi ya gharama za lazima. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita (2021 – 2024), Serikali ilichukua hatua mahsusi nne zifuatazo katika kuwapunguzia gharama wananchi kwa kuondolewa gharama za lazima ambazo wangefanya. Hatua hizi ziliwaokolea wananchi jumla ya ***shilingi 5,724,027,381,324*** ambapo jumla ya wananchi ***11,036,444*** walinufaika moja kwa moja kwa mchanganuo ufuatao:

i) Katika kipindi cha 2020 hadi 2024, Serikali ya CCM ilitumia shilingi ***961,496,032,731*** kama ruzuku iliyotolewa kwa kaya masikini ili kuziwezesha kuongeza kipato cha kaya katika kuzisaidia kaya hizo kumudu gharama za mahitaji ya msingi kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF) na kunufaisha wananchi 5,202,655;

ii) Katika kipindi cha 2020 – 2024, Serikali ya CCM ilitumia shilingi

***693,631,308,093*** kama ruzuku ya mbolea ili kupunguza makali ya bei kwa wakulima, na jumla ya wakulima 2,198,376 walifaidika; na

iii) Katika kipindi cha 2020 – 2024, Serikali ya CCM ilitumia shilingi ***1,308,900,040,500*** katika kuendelea kutoa elimu bila ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita ambapo jumla ya wanafunzi 3,314,198 walinufaika.

iv) Serikali ya CCM ilitumia shilingi ***2,760,000,000,000*** kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ambapo wanafunzi 321,215 walinufaika.

***29.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa maelezo hayo ni wazi kuwa Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa katika kuwawezesha wananchi kiuchumi na huu ni msingi mkubwa wa kuendelea kufanya makubwa zaidi mbeleni. Ni kwa sababu hii sina shaka hata kidogo kwamba katika uchaguzi mkuu ujao wananchi wa Tanzania wanafanya uamuzi sahihi wa kuirudisha CCM na Dkt. Samia Suluhu Hassan madarakani ili kazi iendelee.

***30.*** ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina ya kuhusu tathmini ya utekelezaji kwa mwaka 2024/25 yanapatikana katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2025/26.

***31.*** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa mipango ya serikali niliyoieleza hapo juu, tathmini inaonesha

kuwa wananchi walio wengi wanaridhishwa na utendaji wa serikali katika kutekeleza programu na miradi ya maendeleo. Kwa mfano, utafiti uliofanywa na Taasisi ya Afrobarometer mwezi Juni – Julai 2024 ulionesha kuwa asilimia 71 ya wananchi waliohojiwa walisema wanaridhishwa na utendaji wa serikali, na asilimia 70 walisema nchi ipo katika mwelekeo sahihi. Hii inaonesha kuwa wananchi walio wengi wanaridhishwa na utendaji wa serikali yao.

## MALENGO NA VIPAUMBELE KATIKA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26

***32.*** ***Mheshimiwa Spika*** Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 unaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuwezesha Tanzania kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 na kuwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu. Aidha, Mpango unaopendekezwa ni wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Hivyo, Mpango huu umejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo katika maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

***33.*** ***Mheshimiwa Spika***, Mpango huu ni kiungo kati ya mipango inayokamilika na mipango mipya inayotarajiwa kutekelezwa chini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Hivyo, Mpango huu utajielekeza katika kuainisha na kutekeleza programu na miradi muhimu ambayo haijakamilika ili kuandaa mazingira shirikishi na endelevu kwa mipango ijayo***.***

***34.*** ***Mheshimiwa Spika***, Nguzo muhimu ya maandalizi ya Mpango ni ukuaji wa uchumi pamoja na maeneo matano ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maandalizi ya vipaumbele vya Mpango yamezingatia vigezo vilivyoainishwa kwenye Mpango ambavyo ni: Ukuaji endelevu wa uchumi; kupunguza

umaskini; kuzalisha ajira; kuimarishwa kwa ushindani katika masoko ya kikanda na kimataifa; maendeleo endelevu; utawala bora na utawala wa sheria. Vilevile, Mpango huu unalenga kutekeleza na kukamilisha programu na miradi ya maendeleo ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

***35.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ufanisi wakati wa utekelezaji, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaweka mkazo katika maeneo ya miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa na kujielekeza katika vipaumbele kama ifuatavyo:

i) Kuchochea uchumi shindani na shirikishi
ii) Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani na Utoaji Huduma;
iii) Kukuza Uwekezaji na Biashara;
iv) Kuchochea Maendeleo ya Watu; na
v) Kuendeleza Rasilimali Watu.

***36.*** ***Mheshimiwa Spika*** Ili kufikia vipaumbele vilivyoainishwa Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kielelezo na kimkakati. Baadhi ya miradi itakayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

i. Miradi ya kuongeza uwezo wa uzalishaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ikiwemo ya kuongeza matumizi ya mbegu bora na mbolea, kuongeza eneo la umwagiliaji na kukamilisha ujenzi wa bandari ya uvuvi
ii. Miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usafiri na uchukuzi, pamoja na

miundombinu ya kidigitali kwa ajili ya kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwemo:

a. Kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha cha kimataifa (Standard Gauge Railway – SGR) kwa vipande vilivyosalia
b. Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa uimarishaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)
c. Kuendelea kuboresha na kupanua mtandao wa barabara nchini, hususan zinazounganisha maeneo ya uzalishaji vijijini na masoko
d. Mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi – (EACOP)
e. Kuendelea na upanuzi wa miundombinu ya digitali ili kupanua matumizi ya TEHAMA katika uzalishaji, biashara na utoaji wa huduma kwa wananchi

iii. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha, kusafrisha na kusambaza umeme

iv. Kuendelea na utekelezaji wa miradi inayolenga kuleta maendeleo ya watu ikiwemo: utekelezaji wa sera mpya ya elimu; miadi ya afya; maji na usafi wa mazingira; na

v. Miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji,ili kuhamasisha wawekezaji kutoka nje na kuwawezesha wawekezaji wa ndani ya nchi.

***37.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mafanikio ya utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yatajengwa katika

nguzo na misingi ifuatayo:

i) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi, katika nchi jirani na duniani kwa ujumla;

ii) Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini;

iii) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini;

iv) Kuendelea kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara;

v) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko);

vi) Kuwa na rasilimali watu iliyo bora na inayokidhi matakwa ya sasa ambayo yanatawaliwa na teknolojia na ubunifu;

vii) Nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na udhibiti wa deni la taifa;

viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia wafanyabiashara na wawekezaji wadogo na wa kati ili waongeze tija, wakue na kujirasimisha; na

ix) Kuwa na nidhamu ya utekelezaji wa vipaumbele kama tulivyopanga katika mipango na mikakati ya kitaifa na ya kisekta.

## HITIMISHO

***38.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Nihitimishe kwa kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa kuwa hali ya uchumi wa nchi yetu kwa sasa ni himilivu, ukiwa na mwelekeo chanya na ukuaji endelevu. Kuimarika kwa uchumi kunatokana na usimamizi makini wa sera za uchumi jumla, pamoja na ushiriki wa wananchi wote katika ujenzi wa Taifa. Ninawashukuru na kuwapongeza Watanzania wote kwa mshikamano huu wa kizalendo.

***39.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninapohitimisha, ninaomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kwa uamuzi wao sahihi wa kuwachagua, hapo tarehe 18-19 Januari 2025, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu kuwa mgombea wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa mgombea wake mwenza katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu. Ninaungana na waheshimiwa mawaziri walionitangulia, wabunge na watanzania walio wengi kuwapongeza sana kwa uteuzi wao huo. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya urais wa Zanzibar kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Hakika ***KAZI NA UTU – TUNASONGA MBELE***

***40.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru sana viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango kwa ushirikiano wao katika kuandaa Taarifa ya Hali ya

Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26. Hawa ni **Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo**, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, **Dkt. Tausi Mbaga Kida** (Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji), **Dkt. Fred Matola Msemwa** (Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango), Aidha, ninawashukuru Menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Tume ya Taifa ya Mipango kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

***41.*** ***Mheshimiwa Spika***, kazi ya kuandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi ni kazi shirikishi inayofanywa na wataalam wa Tume ya Taifa ya Mipango na wenzao kutoka Wizara ya Fedha. Aidha, katika mchakato wa kuandaa taarifa hizi mbili tumeshirikiana kwa karibu na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), pamoja na timu yake ya wataalam. Nimashukuru sana yeye binafsi kwa ushirikiano makubwa ambayo tumejenga katika kuhakikisha kwamba majukumu tuliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais tunayakamilisha ipasavyo.

***42.*** ***Mheshimiwa Spika***, kwa umuhimu wa kipekee kabisa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Ubungo kwa ushirikiano wao katika kipindi chote tangu niwe Mbunge wa Jimbo la Ubungo. Aidha, ninakishukuru chama changu (CCM) kwa imani kubwa kilichonipatia ya kupeperusha bendera ya chama kwa mwaka 2020.

***43. Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii pamoja na vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 vinapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji (www.planninginvestment.go.tz ).

***44. Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26.

***45. Mheshimiwa Spika,*** Ninaomba Kutoa Hoja!